*Mulika, Juz. 44(2), 227-247*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Sababu za Kuibuka kwa Uchapishaji-binafsi wa Kazi za Fasihi Andishi ya Kiswahili Nchini Tanzania

*Erasto Duwe*[1], *Angelus Mnenuka*[2], *na Leonard Bakize*[3]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.5

**Ikisiri**

Makala hii inakusudia kubainisha sababu za kuibuka kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili nchini Tanzania. Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani kwa njia ya usaili kutoka kwa wadau mbalimbali wa uchapishaji. Utafiti uliozalisha makala hii uliongozwa na Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi iliyoasisiwa na Everett Rodgers (2003). Aidha, makala hii imetumia mkabala wa kitaamuli katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Kufanyika kwa utafiti wa makala hii kulichochewa na kuibuka na kutamalaki kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili ilhali uchapishaji wa kijadi wa kazi hizo ulioaminiwa na kutumika kwa muda mrefu ukiendelea kutumika. Makala hii imemaizi kuwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili umeibuka na kushamiri katika karne ya 21 kutokana na sababu zifuatazo: wachapishaji kukabiliwa na changamoto za kiuchumi, kutozingatia taratibu za kimkataba, kuteua miswada ya kuchapisha kwa kuzingatia umaarufu wa majina ya waandishi; uchache wa mashirika ya uchapishaji; waandishi kukatishwa tamaa na mlolongo mgumu wa kiuchapishaji, kuombwa au kutengenezewa mazingira ya kuombwa rushwa, kukwepa shinikizo la wachapishaji la kubadili fani na maudhui ya kazi, na kusuasua kwa soko la vitabu vya fasihi nchini Tanzania.

## 1.0 Utangulizi

Utafiti uliozaa makala hii ulichunguza sababu za kuibuka kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili (riwaya, tamthiliya, ushairi na hadithi fupi) nchini Tanzania. Tangu kuanzishwa kwa mashirika ya uchapishaji nchini, kazi nyingi za fasihi zimekuwa zikichapishwa katika mashirika rasmi ya uchapishaji (Suriano, 2020; Reuster-Jahn, 2020). Mashirika hayo ya uchapishaji ya ndani na nje ya nchi yamekuwa yakifanya kazi kwa kuzingatia taratibu maalumu za kiuchapishaji. Taratibu hizo zinawahusisha wadau mbalimbali ambao ni mwandishi, mchapishaji, mpigachapa, msambazaji na msomaji. Katika mtindo huu

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: duweerasto2015@yahoo.com

[2] Profesa Mshiriki, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baruapepe: amnenuka@udsm.ac.tz

[3] Mhadhiri, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baruapepe: leobakize@gmail.com

wa uchapishaji, mwandishi huandika kazi yake na kuiwasilisha kwa mchapishaji ambaye huishughulikia kwa mujibu wa taratibu za kiuchapishaji (Barker, 2020; Phillips na Clark, 2025). Mtindo huu wa uchapishaji unajulikana kama uchapishaji wa kijadi ambapo mchapishaji ndiye mdau mkuu wa shughuli zote za uchapishaji na mwenye mamlaka ya kuamua kuhusu miswada ya kuchapishwa. Kadhalika, mchapishaji ndiye anayelipia gharama zote za uchapishaji wa miswada iliyoteuliwa kuchapishwa. Uchapishaji wa aina hii umekuwa ukiaminiwa na kutumiwa na wadau wengi wa uchapishaji. Kuaminiwa huko kunatokana na uthibitiubora unaotumika katika hatua mbalimbali za uchapishaji na, hivyo, kuwa na uwezekano mkubwa wa kutoa vitabu vyenye ubora unaoridhisha (Carolan na Evain, 2013). Mtindo huu wa uchapishaji umetumika nchini Tanzania tangu karne ya 19 uchapishaji ulipoingizwa na wamisionari (Chachage, 1991; Mulokozi, 2003, 2014).

Hata hivyo, kunako karne ya 20, kuliibuka mtindo mpya wa uchapishaji. Katika mtindo huo, waandishi, baada ya kuandika kazi zao, huzishughulikia wenyewe katika hatua zote (kuhariri, kusanifu, kugharimia upigajichapa, kutangaza na kuuza) ili kutoa vitabu (Hviid na wenzake, 2017; Kumar, 2020). Hata hivyo, kwa kuwa uchapishaji ni taaluma inayohitaji weledi wa aina yake, si rahisi kwa kila mwandishi kumudu kuishughulikia kazi yake katika kila hatua ya uchapishaji. Wakati mwingine, mwandishi huhitaji msaada wa mawakala wa uchapishaji-binafsi ili kufanyiwa baadhi ya shughuli kwa makubaliano ya malipo (Campbell, 2016). Baada ya vitabu kutolewa, mwandishi huvichukua na kuvitafutia soko. Mdau mkuu wa uchapishaji katika uchapishaji-binafsi ni mwandishi mwenyewe. Hivi sasa, waandishi wengi, wakiwamo wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili, hutumia njia hii kuchapisha kazi zao. Uchapishaji wa vitabu wa aina hii unajulikana kama uchapishaji-binafsi.

Nchini Tanzania, uchapishaji-binafsi ulibisha hodi mnamo miaka ya 1960 na kuanza kutumiwa na waandishi wachache sana (Robert, 1991/2018; Mulokozi na Kitogo, 2021). Kundi la waandishi liliibuka na kutumia njia hii ya uchapishaji kunako miaka ya 1970 na 1980 (Kimura, 1990; Mulokozi, 2010) na uchapishaji huu kushamiri mnamo miaka ya 2000. Uchapishaji huo nchini Tanzania unafanywa na mwandishi mmojammoja au baadhi ya waandishi huungana na kusaidiana katika hatua mbalimbali za utoaji wa kitabu cha mwandishi husika kama wanavyofanya wanachama wa Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira (UWARIDI) (Diegner, 2018; Reuster-Jahn, 2020). Licha ya baadhi ya waandishi kuendelea kuchapisha kazi zao za fasihi katika mashirika ya uchapishaji ya kijadi, uchapishaji-binafsi umekuwa kimbilio la baadhi ya waandishi. Idadi ya waandishi wanaochapisha binafsi nchini Tanzania imekuwa ikiongezeka siku hadi siku (Reuster-Jahn, 2017; Mulokozi, 2024). Kwa hiyo, kimahususi makala hii ilichunguza sababu za kuibuka na kushamiri kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za

fasihi andishi ya Kiswahili nchini Tanzania ilhali uchapishaji wa kijadi wa kazi za fasihi ambao umekuwa ukiaminika na kutumika kwa muda mrefu ukiendelea.

Ni vigumu kuzungumzia kuibuka kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi nchini Tanzania bila kugusia uchapishaji wa kijadi ulivyoingia nchini. Ujio wa wageni kutoka nje ya bara la Afrika ndio ulileta uchapishaji nchini Tanzania kama ilivyokuwa katika baadhi ya nchi za Afrika (Chakava, 1996; Mulokozi, 2003; James, 2011). Mulokozi (2003) anaeleza kuwa wamisionari ndio waliotujengea msingi wa uandishi na uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili. Mathalani, hadithi za Waswahili zilianza kuchapishwa mnamo mwaka 1867 na Askofu Edward Steere wa Universities' Mission to Central Africa (UMCA). Mitambo ya awali ya kuchapisha vitabu katika Afrika Mashariki iliingizwa Zanzibar mwaka 1875 na Askofu Steere na kufuatiwa na maeneo mengine kama vile Mombasa mwaka 1887 (Freetown Mission Press), Tabora mwaka 1890 (Taveta Mission Press-TMP) na Tanga mwaka 1905 (Magila Press) (Chachage, 1991; Mulokozi, 2003).

Kukosekana kwa msingi wa uandishi na uchapishaji Afrika Mashariki kabla ya ujio wa wageni, kulisababisha kazi za fasihi ya Kiswahili za awali zilizowahusu watu walioishi kunako karne ya 12-15 zisichapishwe. Badala yake, ziliandikwa na kuchapishwa mnamo karne ya 19 na 20. Miongoni mwa kazi hizo ni kama vile *Utenzi wa Ras al-Ghuli* (Mgeni bin Faqihi), *Utendi wa Fumo Liyongo* (Muhamadi Kijumwa), *Utenzi wa Al-Inkishafi* (Sayyid Abdallah bin Ali) na *Utenzi wa Mwanakupona* (Mwanakupona Binti Mshamu) (Mulokozi, 1999). Baadhi ya tungo hizo zilihifadhiwa katika hati ya Kiarabu na, baadaye kuchapishwa huko Ulaya kunako karne ya 19 na halafu Afrika Mashariki mnamo karne ya 20 baada ya kuimarishwa kwa shughuli za uchapishaji (Mulokozi, 1999; Ngugi, Lyimo na Bakize, 2019). Kunako miaka ya 1920-1940, kazi nyingi za wenyeji zilichapishwa, zikiwamo hadithi mbalimbali kama vile "Mwaka katika Minyororo" (Samuel Sehoza) na "Tulivyoona na Tulivyofanya Ingreza" (Martin Kayamba). Mnamo mwaka 1934, James Mbotela alichapisha kitabu chake cha kwanza kilichoitwa *Uhuru wa Watumwa*[4]. Kuasisiwa kwa East African Literature Bureau (EALB)[5] kunako mwaka 1948, kulirahisisha uchapishaji wa kazi za fasihi ya Kiswahili. Shirika hili liliwezesha uchapishaji wa kazi nyingi za mwanzo za kifasihi kufanyika. Mathalani, kazi za waandishi kama vile Shaaban Robert, Amri Abedi, Mathias Mnyampala, Mohammed S. Abdulla, Henry Kuria, Gershon Ngugi, Graham Hyslop zilichapishwa. Mnamo miaka ya 1950 kazi nyingi za ushairi zilichapishwa. Kati ya kazi hizo ni *Utenzi wa Kutawasifi Nabii* (Hemed bin Abdallah el-Buhriy), *Utenzi wa Vita vya Wadachi Kutamalaki Mrima* (Hemed bin Abdallah el-Buhriy) na *Utenzi wa Vita vya Maji Maji* (Abdul Karim bin Jamalididdini) (Chachage, 1991). Licha ya EALB kuendelea kufanya kazi na,

[4] Hii ni riwaya ya kwanza ya Kiswahili kuchapishwa (Mulokozi, 2017).

[5] Shirika la uchapishaji lililoanzishwa na serikali ya kikoloni ya Afrika Mashariki.

mahitaji makubwa ya kielimu kuibuka nchini, bado shirika hilo halikufanikiwa kuyafikia mahitaji ya waandishi. Uchapishaji wa kazi za fasihi uliendelea pia kufanyika nje ya nchi. Mulokozi (2014) anaeleza kwamba kunako miaka ya 1950-1960, vitabu vingi vya fasihi vilichapishwa huko Ulaya (London) na Afrika Kusini (Witwatersrand). Miongoni mwa mashirika yaliyohusika na uchapishaji wa vitabu wakati huo yalikuwa Evans Brothers, Nelson, Oxford, Sheldon, Longman, Pitman, Macmillan na Collins. Kwa mfano, tamthiliya za *Julius Caesar* na *Mabepari wa Venice* (1963) zilizotafsiriwa na Julius K. Nyerere, zilichapishwa na Oxford University Press. EALB liliendelea kufanya kazi hadi pale lilipovunjwa mwaka 1977, baada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kusambaratika.

Katika kipindi hiki, tayari wamisionari walikuwa wamejistawisha katika maeneo mbalimbali nchini kwa shughuli za uchapishaji. Licha ya kuchapisha vitabu vya mafundisho ya dini na elimu, walichapisha pia vitabu ya fasihi ya Kiswahili, yaani riwaya, tamthiliya, ushairi na hadithi fupi. Kulikuwa na mashirika maarufu ya uchapishaji na upigajichapa ya kidini kama vile Taveta Mission Press (Tabora), Inland Press (Mwanza), Ndanda Mission Press (Mtwara), Rumuli Press (Bukoba), Benedictine Fathers Press (Peramiho), Vuga Press (Tanga), Catholic Publishers (Dar es Salaam), na White Fathers Press (Bukoba) (Chachage, 1991; Mulokozi, 2003).

Kunako mwaka 1965, shirika la East African Publishing House (EAPH) lilianzishwa Afrika Mashariki na Baraza la Utamaduni la Afrika Mashariki. Mulokozi (2014) anafafanua kwamba, licha ya kuchapisha vitabu vya kiada, EAPH lilichapisha pia vitabu vya fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, EAPH lilikoma utendaji wake mnamo mwaka 1987 na kugawanywa rasilimali zake kwa Kenya na Tanzania, hivyo, kukawa na Kenya Literature Bureau (Kenya) na Eastern Africa Publications Ltd (EAPL), Arusha (Tanzania) (Chachage, 1991; Mulokozi, 2014).

Aidha, shirika la Tanzania Publishing House (TPH) lilianzishwa mnamo mwaka 1966 na serikali ya Tanzania baada ya Macmillan kutaifishwa. Serikali ilianzisha pia mashirika mengine ya uchapishaji kama vile Wizara ya Elimu, Dar es Salaam University Press (DUP) na Tanzania Library Service (TLS). Bgoya (1984) anaeleza kuwa mashirika hayo na Eastern Africa Publications Ltd (EAPL) yalikuwa miongoni mwa mashirika makubwa ya uchapishaji nchini Tanzania ambayo, licha ya kuchapisha vitabu vingine, yalichapisha pia vitabu vya fasihi. Hata hivyo, kulikuwa pia na mashirika mengine yaliyokuwa chini ya watu binafsi. Mashirika hayo yote, yaani ya serikali na ya watu binafsi, yaliibuka na kufa kutokana na sababu anuwai, zikiwamo za kiuchumi. Pia, Mradi wa Vitabu vya Watoto (CBP)[6] ulikuwa na mchango mkubwa katika uchapishaji wa vitabu vya

[6] Kifupisho cha Children's Book Project – Mradi wa vitabu vya Watoto ulioanzishwa nchini Tanzania mwaka 1991 na kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 25 kwa madhumuni ya kuchapisha

fasihi andishi ya watoto vya Kiswahili na Kiingereza katika Afrika Mashariki, hususani Tanzania na Kenya. Kwa mfano, nchini Tanzania, kufikia mnamo mwaka 2015, zaidi ya vitabu 350 tofautitofauti, vilikuwa vimechapishwa. Hata baada ya mwaka 2019, bado vitabu vya watoto vimeendelea kuchapishwa (Ngugi, Lyimo na Bakize, 2019). Mashirika yote yaliyojadiliwa katika sehemu hii na mengine kama Mkuki na Nyota Publishers Ltd., Africa Proper Education Network (APE), E & D Vision Publishing, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na Tanzania Educational Publishers (TEPU), yamekuwa yakichapisha kazi za fasihi andishi ya Kiswahili kwa kuzingatia taratibu za uchapishaji wa kijadi.

Kwa upande mwingine, kama ilivyodokezwa hapo awali, kunako miaka ya 1960 kulianza kujitokeza uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi. Chachage (1993) anaeleza kuwa waandishi, Shaaban Robert wa Tanzania na James Mbotela wa Kenya, walipewa masharti magumu na wachapishaji wa vitabu vyao vya fasihi. Baadhi ya masharti hayo ni kwamba, ili vitabu vyao vichapishwe, ilikuwa ni lazima wakubali kununua idadi fulani ya vitabu hivyo. Pamoja na masharti hayo, Chachage anaeleza kuwa waandishi hao walinyonywa na kukandamizwa na wachapishaji hao katika stahiki zao. Kwa sababu hiyo, mwaka 1960 Robert alichapisha binafsi vitabu vyake viwili (Robert, 1991/2018; Mulokozi na Kitogo, 2021). Pia, Chachage (1991), Mulokozi (2010) na Reuster-Jahn (2020) wanaeleza kuwa katika miaka ya 1970 na 1980, baadhi ya waandishi wa fasihi pendwa wa Tanzania walichapisha binafsi kazi zao za fasihi.

Licha ya uchapishaji-binafsi kuanza kutumiwa nchini Tanzania tangu miaka ya 1960 na waandishi wachache (taz. Robert, 1991/2018; Mulokozi na Kitogo, 2021), na baadaye, mnamo miaka ya 1970 hadi 1990, kutumiwa na baadhi ya waandishi wa fasihi pendwa (Chachage, 1991; Mulokozi, 2010; Reuster-Jahn, 2020); katika miaka ya 2000 (Reuster-Jahn, 2008; Gromov, 2014)[7] hadi wakati utafiti huu ukifanyika, mbinu hii ya uchapishaji imepata mashiko zaidi na, imekuwa kimbilio la waandishi wengi wa fasihi andishi ya Kiswahili, chipukizi na wakongwe (Timammy na Habwe, 2022; Mulokozi, 2024). Mathalani, Timammy na Habwe wanaeleza kuwa, sababu ya waandishi wengi kuchapisha binafsi ni wachapishaji wa kijadi kutopokea kazi zao kwa sababu ya uanagenzi wa waandishi na majina yao kutojulikana katika soko la vitabu.

---

vitabu vya watoto, kuratibu usomaji wa vitabu, makongamano, warsha na semina, na kushirikiana na wadau wa vitabu ndani na nje ya nchi.

[7] Licha ya uchapishaji wa kazi za fasihi wa miaka ya 1960-1990 uliotajwa katika makala hii kurejelewa na wataalamu kama uchapishaji-binafsi, utafiti huu umebaini kuwa uchapishaji huo unatofautiana na uchapishaji-binafsi ulioibuka katika miaka ya 2000. Unasibishaji wake unatokana na baadhi ya nduni zake kulingana kiutendaji. Hata hivyo, makala hii imeshughulikia uchapishaji-binafsi ulioibuka katika miaka ya 2000.

Maandiko yaliyoshughulikiwa katika sehemu hii yameonesha kuingia kwa uchapishaji wa kijadi ambao umetumika kama njia kuu ya kuchapisha vitabu, vikiwamo vya fasihi andishi ya Kiswahili. Njia hii imeonesha ufaafu kwa kuwa imewezesha kuchapisha vitabu vya kuridhisha kiubora kutokana na uthibitiubora unaozingatiwa katika mlolongo wa uchapishaji. Hata hivyo, kwa mujibu wa maandiko hayo, kuibuka kwa uchapishaji-binafsi kama ilivyodokezwa hapo awali, kumetokana na sababu mbalimbali kama waandishi kuwekewa masharti magumu na wachapishaji wakati wa kuwasilisha miswada yao, kukandamizwa kwa kutolipwa au kulipwa kidogo mirabaha yao na kutopokea miswada yao kutokana na kutojulikana. Vilevile, baadhi ya maandiko yamebainisha kwamba waandishi wa fasihi pendwa waliamua kuchapisha kazi zao kwa kuwa wachapishaji wa kijadi walikataa kupokea kazi hizo. Hata hivyo, sababu ya kutopokea kazi hizo haijulikani. Sababu zilizotolewa zinahusiana zaidi na uchapishaji-binafsi uliofanyika kunako miaka ya 1960-1990. Kwa hivyo, msukumo wa kufanyika kwa utafiti wa makala hii ulitokana na kiu ya kutaka kubaini sababu za kuibuka na kushamiri kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili nchini Tanzania kunako miaka ya 2000 hadi 2024, licha ya uchapishaji wa kijadi kuendelea kutumika.

## 2.0 Methodolojia ya Utafiti

Data za makala hii zilipatikana kwa mbinu ya usaili kutoka kwa watoataarifa 40 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Ruvuma, Kagera, Arusha na Mjini Magharibi (Zanzibar). Mbinu za usampulishaji lengwa, usampulishaji nasibu taratibishi na usampulishaji tajwa zilitumika kuwapata watoataarifa wachapishaji-binafsi (9), wachapishaji wa kijadi (9), waandishi wanaochapisha katika mashirika ya kijadi (9), wataalamu wa uchapishaji (5), wataalamu wa fasihi (5) na waratibu wa shughuli za uchapishaji wa asasi za serikali (3). Watoataarifa hao waliteuliwa kutokana na kuhusika kwao katika shughuli za uchapishaji wa vitabu. Kwa sababu hiyo, walikuwa na maarifa faafu yaliyohitajika katika kukidhi matakwa ya utafiti wa makala hii. Mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui ilitumika katika kuchambua data. Vilevile, mkabala wa kitaamuli ulitumika katika hatua anuwai za utafiti na ufafanuzi wa data za makala. Kwa sababu za kiitikeli, watoataarifa wametajwa kwa kutumia misimbo.

## 3.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti wa makala hii uliongozwa na Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi (kuanzia sasa, NMU) iliyoasisiwa na Everett Rodgers huko nchini Marekani mnamo mwaka 1962. NMU imefafanuliwa katika kitabu chake cha *Diffusion of Innovations* (2003). Ufafanuzi wa NMU umetolewa pia na wataalamu wengine kama Robinson (2009) anayefasili kuwa uvumbuzi ni wazo, tabia au kitu kinachochukuliwa na wanajamii kuwa ni kipya. Nao Al-Jabri na Sohail (2012) wanaongeza kwamba NMU inabainisha sababu zinazoukilia matumizi ya uvumbuzi katika uga unaohusika na namna uvumbuzi huo unavyotumiwa na watu.

Kimahususi, nadharia hii inahusu jinsi fikra mpya au taratibu fulani mpya za kiutendaji zinavyoenea katika jamii. Katika uchapishaji-binafsi, NMU ina tija kubwa katika kumaizi matumizi ya teknolojia mpya na ueneaji wa uchapishaji-binafsi kati ya waandishi wa vitabu na wasomaji wao. Aidha, NMU kupitia mihimili yake hutumika kubainisha sababu za waandishi kuamua kutumia mbinu mahususi katika uchapishaji wa vitabu vyao. Kwa ujumla, NMU imewezesha kuona namna waandishi, baada ya kukosa nafasi ya kuchapisha kwa wachapishaji wa kijadi, walivyotumia teknolojia kuchapisha wenyewe kazi zao za fasihi.

Nadharia hii inaundwa na mihimili sita ambayo ni: mosi, upatikanaji wa tija hutoa msukumo wa kutumika kwa uvumbuzi mpya. Pili, uvumbuzi mpya aghalabu huelekeana na teknolojia inayotumika katika bidhaa na huduma zilizopo. Tatu, ugumu au urahisi wa kutumia uvumbuzi mpya huweza kutoa msukumo wa kutumia au kutotumia uvumbuzi huo. Nne, uvumbuzi unaojaribika, hutoa uhakika wa kuutumia na kufanikiwa kwa watumiaji tarajali. Tano, kupatikana kwa matokeo chanya ya uvumbuzi mpya huwezesha uvumbuzi huo kuwa na watumiaji wengi. Sita, mustakabali wa bidhaa sokoni au katika matumizi hutegemea mahitaji na thamani au ubora wake. Utafiti wa makala hii umeongozwa na mhimili wa kwanza, wa tatu na wa tano.

## 4.0 Sababu za Kuibuka kwa Uchapishaji-Binafsi

Makala hii imebaini kuwa kuna sababu nane za kuibuka kwa uchapishaji-binafsi nchini Tanzania zinazohusiana na masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na binafsi ambazo ni: changamoto za kiuchumi, mlolongo mgumu wa kiuchapishaji, rushwa, shinikizo la kubadili fani na maudhui ya kazi ya fasihi, ukiukaji wa taratibu za kimkataba na uteuzi wa miswada kwa kuzingatia umaarufu wa majina ya waandishi. Sababu hizo zimejadiliwa katika sehemu hii kama ifuatavyo:

### 4.1 Changamoto za Kiuchumi

Ili mashirika ya uchapishaji yaweze kuchapisha, yanahitaji fedha. Mchapishaji anahitaji kuwa na mtaji utakaomwezesha kuratibu na kuendesha shughuli za uchapishaji (Akidi, 2014). Utafiti wa makala hii umebaini kuwa changamoto za kiuchumi zinazowakabili wachapishaji wengi, ni miongoni mwa masuala yaliyochangia kuibuka kwa uchapishaji-binafsi nchini Tanzania. Ilibainika kuwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi wakati utafiti huu ukifanyika, mashirika ya uchapishaji mengi yamekuwa yakikabiliwa na changamoto za kiuchumi. Changamoto hizo zimechangiwa na masuala mbalimbali. MT1[8] anaeleza:

[8] Mtoataarifa mtaalamu wa uchapishaji aliyesailiwa tarehe 19 Julai 2024.

Data Na. 1

> … huko nyuma katika historia ya uchapishaji Tanzania, wachapishaji wa serikali na wachapishaji wa sekta binafsi walikuwa na uwezo wa kutengeneza vitabu vya shule ambavyo viliuzwa shuleni wakapata faida kubwa. Faida hiyo ndiyo iliwawezesha kutengeneza vitabu vingine kama vile vya fasihi … Kuanzia mwaka 2014 kutokana na mabadiliko ya sera ya elimu nchini Tanzania, wachapishaji wamekuwa na biashara ya kusuasua kiasi cha wengi wao kutoweza kupokea miswada ya waandishi…

Data Na. 1 inaonesha mabadiliko yaliyotokea katika tasnia ya uchapishaji wa vitabu nchini Tanzania. MT1 anabainisha namna mabadiliko hayo yaliyotokana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 yalivyoathiri utendajikazi wa mashirika ya uchapishaji na kujikuta katika kipindi kigumu cha kiuchumi. Ilitanabahishwa kuwa, changamoto za kiuchumi zilizopo katika uchapishaji, zimesababishwa na utekelezaji wa sera hiyo ambapo leo hii vitabu vyote vya kiada vya shule za msingi na sekondari huchapishwa na serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Kabla ya utaratibu huo, kulikuwa na uchapishaji huria wa vitabu vya kiada uliowawezesha wateja kununua vitabu hivyo kutoka kwa mchapishaji yeyote. Soko huria liliwawezesha wachapishaji kujipatia faida kubwa iliyochangia kwa kiasi kikubwa kuendesha shughuli za kiuchapishaji katika mashirika yao, ikiwamo kuchapisha vitabu vya ziada, kama vile vitabu vya fasihi andishi ya Kiswahili, ambavyo havina soko kubwa la kuweza kupata faida ya kuitumia kuvichapisha ikilinganishwa na vitabu vya kiada. Licha ya athari za sera ya elimu, ilibainishwa kuwa masuala mengine yaliyoathiri hali ya uchumi kiuchapishaji ni kushuka kwa thamani ya shilingi na mabadiliko ya sera mbalimbali nchini.

Changamoto ya kiuchumi inayoyakabili mashirika ya uchapishaji nchini, imesababisha yashindwe kujiendesha na kuchapisha vitabu vya fasihi. Hali hiyo ndiyo iliyosababisha wachapishaji kupokea miswada michache ya waandishi wa fasihi au kutopokea kabisa. Matokeo yanayoelekeana na haya, yameelezwa na wataalamu kuwapo katika nchi nyingi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (Ondari-Okenwa, 2007; Oyeyinka, Aganbi na OdonkuleAdebyo, 2016; Makotsi, ht). Oyeyinka, Aganbi na OdonkuleAdebyo wakizungumzia kuhusu uchapishaji nchini Naijeria, wanaeleza kuwa changamoto hiyo inahitaji nguvu ya pamoja ya wadau wa uchapishaji wakiongozwa na serikali ili kuipatia ufumbuzi.

**4.2 Mlolongo Mgumu wa Uchapishaji**

Utafiti wa makala hii umebaini kwamba baadhi ya waandishi hukwepa kuchapisha vitabu vyao kwa wachapishaji wa kijadi kutokana na mlolongo wa uchapishaji kuwa mgumu. Ilifafanuliwa kuwa uchapishaji wa kijadi, kwa kawaida, hutumia mlolongo mrefu (Barker, 2020; Phillip na Clark, 2025). Hata hivyo, ilionekana

kuwa mlolongo huo umefanywa kuwa mgumu na wenye utata mwingi. MT3[9] akifafanua kuhusu ugumu wa mlolongo wa uchapishaji wa kijadi, anaeleza:

Data Na. 2

> … Hata hivyo, urefu wa muda unaotumiwa na mashirika yaliyo mengi unazidi kawaida, vitabu vinacheleweshwa sana kutoka. Unaweza ukapeleka mswada ukafuatilia muda mrefu hata zaidi ya mwaka. Mawasiliano huwa ni magumu. Nenda-rudi zinakuwa nyingi, baadaye unarudishiwa kazi yako. Kwa hiyo, ninaona tu bora niwe nachapisha mwenyewe…

Data Na. 2 inaonesha ugumu wa kuchapisha katika mashirika ya kijadi. MT3 alibainisha kuwa baadhi ya wachapishaji hawatoi taarifa kwa waandishi husika kuhusu hatua zinazoendelea kwa mintarafu ya miswada yao baada ya kuiwasilisha. Waandishi wanapoanza kuifuatilia ndipo, ama hurudishiwa na kuambiwa kwamba haifai au hupewa majibu ya hatua zinazoendelea. Hoja hii ilitolewa na watoataarifa wachapishaji-binafsi na waandishi wanaochapisha katika mashirika ya kijadi 16 (88.8%), suala linaloashiria ukubwa wa tatizo. MT5[10] alieleza kuwa mswada wake ulichukua miaka mitano na MT6[11] miaka kumi tangu kuwasilishwa hadi kuchapishwa ilhali MT7[12] mswada wake ulikaa kwa mchapishaji kwa miaka minne kwa ajili ya kutathminiwa na baadaye akarudishiwa akielezwa kuwa hauna sifa za kuchapishwa.

Kwa upande mwingine, hoja kuhusu mlolongo mrefu wa uchapishaji ilitolewa na MT4[13] aliyekiri kuwa mchakato wa uchapishaji ni mrefu kiutendaji na kwamba unawakatisha tamaa baadhi ya waandishi. MT4 alibainisha kwamba muda mrefu unaotumiwa, unatokana na hatua anuwai za kitaalamu zinazopaswa kuzingatiwa. Alikiri kuwa wao ni wafanyabiashara wanaotaka kazi zao zichapishwe kwa ubora ili ziweze kupata soko. Alisisitiza kuwa wachapishaji hufanya kazi kwa umakini mkubwa. Katika Data Na. 3 anaeleza:

Data Na. 3

> Kabla ya kuamua kuteua mswada wa kuchapishwa, kwanza, mswada huo hufanyiwa tathmini na mhariri wa ndani. Pili, bodi ya shirika

[9] Mtoataarifa mchapishaji-binafsi aliyesailiwa tarehe 17 Agosti 2024.

[10] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika ya kijadi aliyesailiwa tarehe 8 Julai 2024.

[11] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika ya kijadi aliyesailiwa tarehe 18 Agosti 2024.

[12] Mtoataarifa mwandishi-binafsi aliyesailiwa tarehe 20 Septemba 2024.

[13] Mtoataarifa mchapishaji wa kijadi aliyehojiwa tarehe 9 Agosti 2024.

> huupitia. Tatu, mswada husika hutumwa kwa wasomaji wa nje ambao lazima wawe wabobevu katika eneo husika la maudhui ya mswada. Wasomaji wanatumia muda mrefu kusoma miswada hiyo. Wasomaji hao wataandika ripoti itakayojibu maswali ikiwa mswada huo unafaa kuchapishwa kitabu… Wakionesha kuwa unafaa, mswada utatakiwa kupelekwa kwa mwandishi ili auboreshe. Kama haufai, mwandishi atarudishiwa mswada wake…

Data Na. 3 inathibitisha madai ya MT3 (rej. Data Na. 2) kuhusu ugumu wa mlolongo wa uchapishaji wa kijadi. Hata hivyo, kwa maelezo ya MT4 (rej. Data Na. 3), urefu wa mlolongo huo wa kiuchapishaji hufanywa kwa nia ya kuhakikisha kazi inatoka ikiwa bora au ya kuridhisha, tofauti na mtazamo wa baadhi ya waandishi wanaoona kuwa mlolongo huo huwachelewesha.

Utafiti wa makala hii unaona kuwa, ugumu wa mlolongo unaolalamikiwa na waandishi hata baadhi yao kupata msukumo wa kuchapisha binafsi kazi zao, unatokana na sababu kadhaa. Mosi, kukosekana kwa mawasiliano baina ya wachapishaji na waandishi. Pili, baadhi ya wachapishaji kuwa na miswada mingi inayosubiri kushughulikiwa. Tatu, uhaba wa wataalamu katika mashirika na, nne, changamoto za kiuchumi zinazoyakabili mashirika. Kwa maoni ya utafiti huu, licha ya changamoto zinazowakabili baadhi ya wachapishaji, kubaki na miswada ya waandishi kwa ajili ya tathmini kwa zaidi ya miaka mitatu au kwa ajili ya kuichapisha bila mawasiliano, ni suala linaloenda kinyume na kaida za uchapishaji kama Komech na Magara (2018) wanavyoeleza kuwa mawasiliano chanya baina ya mwandishi na mchapishaji hujenga uhusiano unaoleta tija katika uchapishaji ilhali kinyume chake huzua hali ya suitafahamu. Uchambuzi wa data za makala hii umemaizi kuwa, licha ya mlolongo wa uchapishaji wa kijadi kuwa mrefu kwa asili, ukosefu wa uwajibikaji kwa baadhi ya wachapishaji hufanya mlolongo huo uonekane kuwa mgumu na wenye utata mwingi kwa waandishi.

### 4.3 Rushwa

Ilibainika kwamba rushwa hutumika katika baadhi ya mashirika ya uchapishaji ili kutoa ridhaa kwa waandishi kuchapisha vitabu vya fasihi. Katika baadhi ya mashirika ya uchapishaji, kuna wafanyakazi wasio waaminifu ambao huomba rushwa au hutengeneza mazingira ya kuomba rushwa kwa waandishi, pindi wanapowasilisha miswada yao ili ifikiriwe kuchapishwa. Ilielezwa na baadhi ya watoataarifa waandishi kuwa waliombwa rushwa na kusumbuliwa kwa kiasi kikubwa. Kama wangetimiza sharti hilo, miswada yao ingependekezwa kuchapishwa kwa kuandikiwa ripoti zenye sifa nzuri kuhusu miswada yao kwa viongozi wa juu wa mashirika husika. Kadhia hiyo hiyo ilitokea wakati wakiwasilisha miswada yao katika mashirika ya uchapishaji.

Ilitanabahishwa na MT8[14] kuwa, alipowasili katika shirika la uchapishaji, alikutana na mhusika aliyepokea mswada wake na kuahidi kuushughulikia kwa mujibu wa taratibu. Hata hivyo, baada ya kuondoka, ilipita miezi mitano bila kujulishwa chochote. Ukimya uliokuwapo, ulimfanya arudi katika shirika hilo kufuatilia ili kujua kilichokuwa kikiendelea. Alipofika, aliambiwa na mhusika kuwa bado mswada huo ulikuwa ukishughulikiwa. Alitakiwa aendelee kusubiri. Akaahidiwa kuwa angejulishwa muda mfupi baada ya kazi kukamilika. Baada ya kuondoka, ilipita miezi mitatu bila taarifa yoyote. Ilimpasa kufuatilia tena. Alipoonana na mhusika na kudadisi kuhusu maendeleo ya kazi yake, MT8 aliambiwa:

Data Na. 4

> … Mpaka leo hujaelewa tu mzee? Wewe ni mtu mzima, usichoelewa ni nini? Ongea kwa herufi kubwa; usiwe na maneno mengi bila vitendo... Vipi, unakuwa kama huelewi? ...

MT8 alieleza kuwa alishtushwa sana na maelezo ya mfanyakazi huyo wa shirika la uchapishaji ambayo hakuyatarajia, kwa masikitiko makubwa alieleza:

Data Na. 5

> Nilishangaa sana, mtu yuko huru katika ofisi ya shirika anaongea kwa uhuru masuala ambayo ni kinyume kabisa na taratibu za nchi kama taasisi hiyo ni ya kwake…

Data Na. 5 inaoneha mshangao na malalamiko ya mwandishi kutokana na hali ambayo hakuitarajia ya kumtaka atoe rushwa ili kupitisha mswada wake. Suala kama hilo lililimtokea pia MT9[15] aliyeombwa rushwa ya shilingi milioni moja katika shirika lingine ili mswada wake upendekezwe kuchapishwa. MT8 alibainisha kuwa hali hiyo ilimpa wazo la kwenda kujaribu kuchapisha binafsi kitabu chake badala ya kuendelea kusumbuliwa.

Kiutaratibu, miswada huteuliwa kuchapishwa kwa kigezo cha ubora wake na taratibu nyingine za mashirika ya uchapishaji (Jolly, 2009). Ni kinyume cha kaida za kiuchapishaji kuteua miswada kwa mlango wa rushwa. Kama inavyofahamika, rushwa ni adui wa haki. Tume ya Pamoja ya Fedha (2021) inabainisha kuwa rushwa huwanyima haki wanajamii na kuchochea ukandamizaji. Tukio hili linaibua taswira hasi kwa baadhi ya mashirika. Suala hili linaashiria kuwa baadhi ya mashirika ya uchapishaji hayazingatii maadili ya kiuchapishaji (Balig, 2017;

[14] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika aliyehojiwa Dar es Salam tarehe 8 Agosti 2024.

[15] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika aliyehojiwa tarehe 17 Julai 2024.

Ahuja na Baishya, 2024). Matokeo haya yanaelekeana na mawazo ya wataalamu kama vile Campos na Pradhan (2007), Ronning (2009) na Bhosale (h.t.). Mathalani, Ronning anaeleza kuwa baadhi ya wafanyakazi katika mashirika ya uchapishaji huomba rushwa kwa sababu ya tamaa au kujiongezea kipato binafsi. Katika muktadha kama ulioelezwa, ni rahisi kuteua kazi zilizo chini ya kiwango na kuacha kazi zenye ubora.

### 4.4 Shinikizo la Kubadili Fani na Maudhui ya Kazi

Fani na maudhui ni vipengele muhimu vinavyoijenga kazi ya fasihi. Utafiti huu ulimaizi kwamba, baada ya waandishi kuwasilisha miswada katika mashirika ya uchapishaji na wachapishaji kuridhia kuichapisha, mara kadhaa, hali ya suitafahamu huibuka baina yao kuhusiana na baadhi ya vipengele vya fani na maudhui ya kazi husika. Ilielezwa kwamba msanii anaweza kuiunda kazi yake ikawa na ujumbe au vipengele fulani vya kifani. Kwa sababu moja au nyingine, mchapishaji anaweza kutaka mswada huo ufanyiwe marekebisho katika baadhi ya vipengele vya maudhui, fani au vyote ilhali msanii wa kazi husika haafiki kufanya hivyo. Ilifafanuliwa na MT10[16] kuwa wakati mwingine mchapishaji huweza kuingilia fani na/au maudhui ya kazi ya fasihi. Mara nyingi migogoro huibuka baina ya wachapishaji na waandishi katika maudhui ya kazi za fasihi. Mchapishaji huweza kulazimisha maudhui fulani mapya yaingizwe katika kazi, yaboreshwe au yaondolewe. MT10 anatanabahisha:

Data Na. 6

> … wakati mwingine hutokea mwandishi anataka dhamira fulani iwepo katika kitabu chake lakini mchapishaji haitaki dhamira hiyo – anataka iondolewe au isichapishwe katika kitabu kinachotarajiwa kuchapishwa

Maelezo ya MT10 katika Data Na. 6 hapo juu, yanalandana na maelezo ya MT11[17] anayebainisha kuwa baadhi ya wachapishaji huwashinikiza waandishi bila kuwaeleza sababu za msingi za kufanya hivyo. Tofauti na MT10 katika Data Na. 6 anayezungumzia maudhui, MT11 katika Data Na. 7 anaeleza kuwa baadhi ya wachapishaji hao huingilia hata vipengele vya kifani. Hapa anaeleza:

Data Na. 7

> Wachapishaji wengine wanaleta ubabe wa kiuchapishaji… wanaondoa msamiati wako wanaweka wao… wanafanya hivyo kwa kuwa wanasema wanaogopa rungu la serikali kwa maudhui ya mtindo fulani na msamiati…

[16] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika aliyehojiwa tarehe 18 Agosti 2024.

[17] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika aliyehojiwa tarehe 18 Agosti 2024.

Data Na. 6 na 7 zinabainisha kile kinachoitwa shinikizo la wachapishaji kwa waandishi, wakitaka baadhi ya vipengele vya fani na/au maudhui vibadilishwe. Ilielezwa kwamba suala hilo huwapa shida waandishi kwani wangependa kazi zao, licha ya kuhaririwa, zibaki na uasili wa uandishi wao kifani na kimaudhui. Utafiti wa makala hii umebaini kuwa shinikizo hilo hutoa msukumo kwa baadhi ya waandishi kuamua kuchapisha binafsi kazi zao za kifasihi kwa lengo la kukwepa athari za wachapishaji katika vipengele hivyo.

Hata hivyo, MT12[18] alifafanua kwamba, mwandishi anapokutana na ushauri wa mchapishaji kuhusu fani na maudhui, anatakiwa kuutathmini ili aone tija yake, badala ya kuona kuwa ni shinikizo. Alieleza kuwa aliwahi kupewa ushauri wa kubadilisha baadhi ya vipengele vya kifani katika kazi yake. Kwa kuzingatia ushauri huo, kazi hiyo ilibadilika na kuwa na ujumi ulioleta mvuto wa kipekee, kuliko ilivyokuwa awali. Kwa maoni ya makala hii, fasiri ya muktadha kama huu ni kuwa, utaalamu wa kuunda kazi ya kifasihi hutofautiana, kwani kuna kuzidiana kimbinu. Kuna wakati mawazo na ufundi wa mwandishi huweza bora lakini huweza pia kuwa kinyume chake na wakati mwingine mawazo ya mhariri wa kimaudhui wa shirika la uchapishaji au mchapishaji yanaweza kuwa bora zaidi kuliko ya mwandishi au kinyume chake. Hivyo, mwandishi na mchapishaji, wanahitaji kuketi mezani, kueleweshana na kukubaliana, ili kufikia mwafaka.

Hali ya kutokukubaliana baina ya mchapishaji na mwandishi kuhusu fani na/au maudhui ya kazi, humsukuma mwandishi kuchapisha kazi yake. Hata hivyo, ilionekana kuwa si kila mchapishaji anayetoa ushauri huo hufanya hivyo kwa masilahi yake. Kwa maoni ya utafiti wa makala hii, wachapishaji wengi hutoa ushauri kama huo kwa matilaba ya kujenga ujumi wa kazi husika au kuthibiti maadili ya kazi hizo kwa kuzingatia taratibu za nchi na miiko ya jamii. Matokeo haya yanaelekeana na mawazo ya watafiti anuwai kama Komakech na Magara (2018), Osadci-Baciu na Zbuchea (2023) na Schroff (2024) ambapo Baciu na Zbuchea wanaeleza kuwa mivutano baina ya waandishi na wachapishaji ni jambo la kawaida ila kinachotakiwa ni kushauriana kwa hoja ili kufikia mwafaka.

### 4.5 Ukiukaji wa Taratibu za Kimkataba

Mara baada ya mchapishaji kuamua kuchapisha mswada wa kazi ya fasihi, makubaliano huingiwa baina yake na mwandishi. Makubaliano hayo huwa katika mkataba wa kimaandishi unaobainisha haki na wajibu wa pande zote mbili, yaani kati ya mwandishi na mchapishaji. Kati ya haki za mwandishi ni kupewa stahiki zake, ukiwamo mrabaha, utokanao na mauzo ya kitabu husika. Utafiti wa makala hii ulibaini kuwa sababu mojawapo ya waandishi kuamua kuchapisha binafsi vitabu vyao vya fasihi, ni wachapishaji kukiuka makubaliano ya kimkataba katika masuala mbalimbali. Miongoni mwayo, ni kutowalipa waandishi stahiki zao,

[18] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika aliyehojiwa tarehe 9 Julai 2024.

kuchapisha vitabu vingi tofauti na makubaliano na kupoteza miswada ya waandishi. MT9 anatanabahisha:
Data Na. 8

> Tangu kitabu changu kilipochapishwa, sikuwahi kupewa mrabaha wangu hadi nilipofuatilia baada ya miaka minne kupita. Nilipodai haki yangu, nilipewa mrabaha wa muda huo ambao ulikuwa shilingi elfu kumi na tano tu… baadaye ilipita tena miaka miwili sikuwekewa. Nilipofuatilia nikaingiziwa shilingi mia nane hamsini tu…

Data Na. 8 inaonesha malalamiko ya wadau dhidi ya wachapishaji kuhusiana na kukosekana kwa uaminifu. Ilitanabahishwa pia na MT13[19] kuwa, baadhi ya wachapishaji hujiamulia mambo mbalimbali kuhusu kazi za waandishi, bila kuwashirikisha. MT13 alieleza kuwa aliandika kazi ya fasihi ya watoto na kumkabidhi mchapishaji ambaye alichapisha vitabu vingi na kuviuza. Ilifafanuliwa kuwa mchapishaji huyo, kwa makubaliano na mchapishaji mwingine wa Kenya, walichapisha vitabu vingine vilivyouzwa nchini Kenya, bila taarifa wala stahiki kwa mwandishi. Suala hilo ni kinyume na kaida za kiuchapishaji na, linachukuliwa kuwa ni aina ya uharamia (Begum na Sharma, 2018; Rastogi, Vivek na Rajpoot, 2024). Hapa MT13 anaeleza:
Data Na. 9

> Mchapishaji fulani alichapisha vitabu vyangu... Mswada wa kitabu hicho aliupeleka vilevile kwa mchapishaji wa Kenya, akalipwa fedha nyingi. Mimi niliyeandika sikulipwa kitu. Nilipogundua na kumtaarifu mchapishaji wa Kenya kuhusu malipo ya vitabu vyangu hivyo, alinijibu kwamba nimtafute mchapishaji wa Tanzania... Mpaka mwisho sikupata chochote!

Data Na. 9 inabainisha changamoto zinazowakabili baadhi ya waandishi wa kazi za fasihi wa Tanzania. Suala la waandishi kutolipwa stahiki zao na kutoshirikishwa katika maamuzi muhimu ya kazi zao (rej. Data. Na. 9), linaashiria unyonyaji na ukandamizaji kwa waandishi; ni kinyume na maadili ya kiuchapishaji yanayomtaka mchapishaji kuwajibika kwa mwandishi (Balig, 2017; IMSTE, 2018[20]; Ahuja na Baishya, 2024). Utafiti huu ulimaizi kuwa, ukiukaji wa taratibu za kimkataba, ni miongoni mwa sababu kubwa zinazowasukuma waandishi kuchapisha binafsi kazi zao. Moja ya matarajio makubwa ya waandishi, licha ya kuwasilisha maudhui wanayoyakusudia kwa hadhira, ni kupata mrabaha utakaowawezesha kukidhi mahitaji yao (Baverstock na Steinitz, 2019). Suala kama hili, la ukiukaji wa makubaliano ya kimkataba, linajitokeza pia katika baadhi ya

[19] Mtoataarifa mwandishi anayechapisha katika mashirika ya kijadi aliyesailiwa tarehe 24 Julai 2024.

[20] *International Society of Managing and Technical Editors*.

nchi za Afrika kama inavyobainishwa na Kenneth (2013) huko Nigeria ambaye anasisitiza umuhimu wa waandishi kujua sheria za kiuchapishaji ili kulinda haki zao.

### 4.6 Uteuzi wa Miswada kwa Kuzingatia Majina ya Waandishi

Utafiti wa makala hii ulibaini hali ya kuwapo kwa upendeleo unaotolewa na baadhi ya wachapishaji kwa waandishi nguli, ambao hutambulika pia kwa lakabu ya 'waandishi wenye majina'. Ilionekana kuwa mswada unaowasilishwa katika shirika la uchapishaji ukiwa na jina la mwandishi mwanagenzi, huchukua muda mrefu kufikiriwa kuchapishwa, tofauti na mwandishi nguli ambaye kazi yake hupewa kipaumbele. MT14[21] anaeleza:

Data Na. 10

> … Sisi waandishi chipukizi tunakabiliwa na changamoto kubwa. Kazi zetu hazikubaliwi na wala hazipewi kipaumbele na wachapishaji kama za waandishi wenye majina makubwa tayari sokoni…

Data Na. 10 inadhihirisha hali ya kuwapo kwa upendeleo wa baadhi ya wachapishaji kwa waandishi 'wenye majina', jambo linalowafanya waandishi wanagenzi waone kama wanabaguliwa. Ilibainishwa na MT14 kuwa hali hiyo huwakatisha tamaa waandishi wanagenzi. Kwa upande mwingine, MT4 alieleza kuwa ni kweli kwamba wachapishaji huwarudishia waandishi miswada yao hasa inapokuwa haiendani na vigezo vinavyotumika katika uteuzi kulingana na taratibu zao. MT4 alifafanua:

Data Na. 11

> Hatupokei tu na kuchapisha mswada wa kila mwandishi. Tunatumia vigezo tulivyojiwekea. Baadhi ya vigezo tunavyoangalia ni: soko, yaani kama kazi husika itapata soko endapo tutaichapisha; pili, uasili wa kazi, katika kigezo hiki tunaangalia kama kazi husika ilivyo ndivyo inatakiwa kuwa… Tatu, tunaangalia ubora wa kazi… Nne, tunaangalia wasifu wa mwandishi kama alishawahi kuchapisha vitabu vingine. Tano, je, mswada umekuja kwa wakati wake?... Tunafanya hivyo kwa lengo la kuhakikisha kuwa gharama zetu za uchapishaji zinarudi... Vinginevyo ni hasara…

Data Na. 11 inaonesha vigezo ambavyo wachapishaji huvitumia kwa ajili ya kuteua miswada ya waandishi ya kuichapisha. Hoja ya uteuzi wa miswada kwa kuzingatia majina ya waandishi ilitolewa na watoataarifa wachapishaji-binafsi 8 (88.8%) na watoataarifa waandishi wanaochapisha katika mashirika ya kijadi 4 (44.4%). Kwa upande mwingine, MT15[22], licha ya kukubaliana na MT14 katika

[21] Mtoataarifa mchapishaji-binafsi aliyesailiwa tarehe 10 Julai 2024.

[22] Mchapishaji wa kijadi aliyesailiwa tarehe 11 Julai 2024.

maelezo yake (rej. Data Na. 11), alikiri kwamba kwa kuwa wao ni wafanyabiashara, wakati fulani huvutiwa na miswada ya waandishi nguli ambao ni wabobevu kiusanii na huwarahisishia kazi. Hivyo, huipa kipaumbele miswada yao kuliko ya waandishi wanagenzi.

Wazo linalofanana na hili linatolewa na Kobia (2006) na Timmamy na Habwe (2022) wanaoeleza kwamba, baadhi ya wachapishaji wa kazi za fasihi nchini Kenya, huteua miswada ya kazi za fasihi kwa kutoa kipaumbele kwa waandishi maarufu, wakiwaacha waandishi chipukizi. Kwa sababu hiyo, waandishi hao chipukizi huamua kutafuta njia za kujichapishia kama Timmamy na Habwe (2022) wanavyoeleza kuwa washairi wa mwambao wanapokosa wachapishaji huamua kuchapisha kwa kutumia simu tamba. Utafiti huu unatoa indhari kuwa wachapishaji wanaotumia kigezo cha kuangalia majina ya waandishi kuteua miswada, wakumbuke jukumu lao la msingi na la asili la kuwalea waandishi wanagenzi (Chachage, 1993; Mulokozi, 2003) na kuipima miswada ya kazi za kisanaa kwa sifa za ubora.

**4.7 Uchache wa Mashirika ya Uchapishaji Nchini**

Sababu mojawapo ya kuibuka kwa uchapishaji-binafsi nchini Tanzania ni uhaba wa mashirika ya kuchapisha kazi za waandishi. Ilibainika kwamba mashirika ya uchapishaji yaliyo hai nchini Tanzania ni machache tofauti na ilivyokuwa kunako miaka 15 iliyopita (taz. Bgoya, 1986; Chachage, 1991; Noromba, 2007; Mulokozi, 2003, 2024). Ilifafanuliwa kuwa mashirika mengi ya uchapishaji yamedorora kiutendaji na mengine yamekufa, hali iliyosababishwa na sababu za kisiasa, kiuchumi na kijamii huku mabadiliko ya sera ya elimu na mafunzo yakitajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa (rej. Data Na. 1). MT16[23] anafafanua:

Data Na. 12

> Suala la waandishi kujichapishia wenyewe linachangiwa na uchache wa wachapishaji wa kazi zao. Mashirika mengi ya uchapishaji yamekufa kutokana na masuala ya kisiasa na kiuchumi. Wachapishaji waliopo wanahesabika, tena, hawawezi kuchapisha kazi nyingi…

Data Na. 12 inaonesha uhaba wa wachapishaji nchini Tanzania katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2024. Hata hivyo, ilibainishwa kuwa mashirika machache yaliyopo nchini yanakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwamo ya kiuchumi. Hali hiyo husababisha mashirika hayo yapokee miswada michache na kuifanyia kazi, na kwamba, ufinyu wa bajeti unaoyakabili, wakati mwingine, huathiri ubora wa kazi zinazochapishwa kwa baadhi ya mashirika. Hoja hii ilibainishwa na watoataarifa 34 (85%), jambo linaloweza kufasiriwa kuwa uchache

[23] Mtoataarifa mtaalamu wa uchapishaji aliyehojiwa tarehe 24 Julai 2024.

wa mashirika ya uchapishaji unachangia kwa kiasi kikubwa kutoa msukumo kwa waandishi kuchapisha binafsi kazi zao.

### 4.8 Kusuasua kwa Soko la Vitabu vya Fasihi ya Kiswahili

Ilibainika kuwa, nchini Tanzania, soko la vitabu vya fasihi linasuasua. Hali hiyo huwafanya wachapishaji wa vitabu wachukue hadhari wakati wa kupokea miswada ya kazi za fasihi. MT15 alifafanua kwamba, kwa kuchelea kupata hasara, wao hupokea miswada michache sana. Ilielezwa kuwa kusuasua kwa soko la vitabu vya fasihi huchangiwa na kukosekana kwa utamaduni wa usomaji nchini. MT14 anaeleza:

Data Na. 13

> Si watu wengi wenye mapenzi ya kusoma vitabu, kwa sababu hiyo havinunuliwi. Katika jamii za shule, hasa kwa wanafunzi, ikitokea mmoja amenunua nakala moja au mbili za kitabu... kitakachofuata ni kuazimana kitabu hicho hadi kitachakaa... Watu wengine hawanunui vitabu…

Data Na. 13 inabainisha ugumu wa soko la vitabu nchini. Akizungumzia hoja hiyo, MT18[24] alieleza kuwa maktaba za umma zimejaa vitabu lakini mara nyingi hazina wasomaji. Maelezo hayo yanaashiria hali duni ya usomaji wa vitabu nchini. Kukosekana kwa utamaduni wa usomaji husababisha ukosefu wa ari ya kununua vitabu. Jambo hilo linawaathiri wachapishaji kimapato na, hivyo, kusababisha uendeshaji na utendaji wa mashirika kudorora au baadhi kufa. Maelezo haya yanashadidiwa na Gaikwad (2020) anayebainisha kuwa biashara huukiliwa na soko lake ilhali soko hilo likiwa duni, biashara hiyo hufanyika kwa kusuasua au hukwama kabisa. Matokeo yanayofanana na haya yanabainishwa na wataalamu kama Makotsi (h.t.) na Kobia (2006) kutokea katika nchi nyingine za Afrika. Kwa mfano, Kobia anabainisha kuwa kama vitabu havipo katika mfumo wa elimu, hasa shule za msingi na sekondari, ni nadra kupata mauzo ya kutosha.

## 5.0 Mjadala Mfupi

NMU imekuwa na athari kubwa kwa waandishi (wachapishaji-binafsi) na data za utafiti huu zilizobainisha sababu za kuibuka kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili nchini Tanzania. Kuwapo kwa vifaa vya kisasa, maarifa mapya na mbinu mpya za kiuchapishaji zilizotokana na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia, ambazo waandishi au mawakala wao, wanaweza kuzitumia kuchapisha kazi za kifasihi, kumetoa msukumo mkubwa kwa waandishi hao kutokata tamaa pale walipokosa nafasi za kuchapisha katika mashirika ya kijadi. Msukumo huo umejengwa katika tija ya kutekeleza matakwa yao ya kuchapisha ili kufikisha mawazo yao kwa jamii na kujipatia kipato kama

[24] Mtoataarifa kutoka asasi ya serikali aliyesailiwa tarehe 16 Julai 2024.

mhimili wa kwanza wa NMU unavyoeleza kuwa, upatikanaji wa tija hutoa msukumo wa kutumika kwa uvumbuzi mpya. Aidha, kama MNU inavyobainisha kuhusu ugumu au urahisi wa kutumia teknolojia mpya (mhimili wa tatu), wachapishaji-binafsi waliona inawezekana kwao (ni rahisi) kutumia teknolojia mpya na kupata matokeo chanya (mhimili wa tano) kuweza kuchapisha. Hivyo, kutofanikiwa kuchapisha katika mashirika ya uchapishaji ya kijadi, hakikuwa kikwazo cha kuwakwamisha moja kwa moja kuchapisha, bali, mbinu mpya zinazotokana na uvumbuzi mpya kama NMU inavyobainisha, zilichochea msukumo na ari ya kuchapisha kazi zao za kifasihi.

**6.0 Hitimisho**

Data zilizowasilishwa katika makala hii zimeonesha sababu mbalimbali za kuibuka kwa uchapishaji-binafsi wa kazi za fasihi andishi ya Kiswahili nchini Tanzania. Utafiti huu ulimaizi kuwa, sababu zilizobainika zinahusiana na sera za nchi, mifumo ya kiuchumi, mifumo ya uchapishaji na taratibu za wachapishaji, ufisadi na kukosekana kwa utamaduni wa usomaji. Sababu hizo zinaonesha kuwa, kwa kiwango kikubwa, waandishi wanaamua kuchapisha binafsi kutokana na mazingira magumu wanayokutana nayo katika harakati za kutafuta wachapishaji wa kazi zao. Kwa ujumla, makala hii imechangia maarifa kuhusu sababu za waandishi kuamua kuchapisha binafsi katika kipindi cha kuanzia mnamo mwaka 2000 hadi 2024, tofauti na sababu zilizobainishwa na tafiti tangulizi.

**Marejeleo**

Ahuja, V.K. na Baishya, K. (2024) *Research and Publication Ethics.* Kamrum: Routledge Resource Centre.

Akidi, J.O. (2014) "Publishing and Printing Business". Katika C.P. Uzuegbu na M.C. Nwosu (Wah.) *Entrepreneurship Studies and Practices in Library and Information Science.* Lagos: Zeh Communication.

Balig, S. (2017) "Publication Ethics and Etiquette: The Golden Commandment". *Journal of Indian Society of Pedodontics and Preventive Dentistry,* Juz. Na. 35(3): 187. DOI: 10.4103/JISPPP 216-17.

Barker, D. (2020) "The Structure and Workings of a Publishing House". Inapatikana katika https://www.taylorfrancis.com. Ilisomwa tarehe 18 Agosti 2024.

Baverstock, A. na Steinitz, J. (2019) "What Makes a Writer? How Do Early Influences Shape, and Working Habits Develop those who Write?" *Publishing Research Quarterly*, Juz. Na. 35(2). DOI: 10.1007/s12109-019-0966-w.

Begum, I. na Kr. Sharma, H. (2018) "Piracy: A Threat to Academicians and Publishers". *Journal of Intellectual Property Rights,* Juz. Na. 23: 261-269.

Bgoya, W. (1984) *Books and Reading in Tanzania*. Paris: UNESCO.

Bgoya, W. (1986) *Books and Reading in Tanzania*. (h.m.). UNESCO.

Bhosale, J. (h.t.) "My Experience with Corruption and Cruelty from Publishing Industry." Inapatikana katika juliebhosale.co.nz. Ilisomwa tarehe 11 Novemba 2025.

Campbell, D. (2016) "Ten Trends Driving the Future of Book Publishing". Inapatikana katika Dugcampbell.com. Ilisomwa tarehe 25 Agosti 2024.

Campos, J.E. na Pradhan, S. (2007) *The Many Faces of Corruption.* Washington DC: World Bank.

Chachage, C.S.L. (1993) "Kiungo Dhaifu kati ya Mwandishi na Jamii". Katika M.M. Mulokozi na C.G. Mung'ong'o (Wah.) *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam: DUP. kur. 19 – 29.

Diegner, L. (2018) "Good-Bye, Book – Welcome, App? Some Observations on the Current Dynamics of Publishing Swahili Novels". *Africa Today*, Juz. Na. 64(4): 31. DOI: 10.2979/africatoday.64.4.03.

Gaikwad, J. na Yadav, B. (2020) "The Significance of Market Research in Business Decision." *Journal of Global Economy*, Juz. Na. 16(2): 11-17. DOI: 10.1956/jge.v1612.650. Ilisomwa tarehe 25 Machi 2025.

Gromov, M.D. (2014) "The Present State of Swahili Literature as an Artistic and Social Phenomenon." *Journal of Language, Technology and Entrepreneurship in Africa*, Juz. Na. 5(1): 30-41.

Hviid, M., Jacques, S. na Sanchez, S.I. (2017) "From Publishers to Self-Publishing: The Disruptive Effects of Digitalisation on the Book Industry". CREATe Working Paper Series DOI: 10.5281/zenodo.321609.

IMSTE (2018) *Publishing Ethics 101 A Guide for Editorial Office*, Toleo la 2. (h.m.). Professional Development Education Committee.

James, I.J. (2011) "Problems of the Publishing Industry in Nigeria: The Oboninje Publishers Experience after 50 Years". *PNL Quarterly*, Juz. 75(3). Inapatikana katika https://www.pnl.org. Ilisomwa tarehe 01 Juni 2024.

Jolly, G.S. (2009) *Book Publishing Management*. New Delhi: Har-Anand Publications Ltd PVT.

Kenneth, T.A. (2013) "Legal Issues in Print and Publishing in Nigeria". *International Journal of Development and Sustainability*, Juz. Na. 2(4) 2368-2382.

Kimura, E. (1990) *Mabadiliko ya Kijamii na Riwaya ya Upelelezi Tanzania*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kobia, M.J. (2006) "Matatizo Yanayowakumba Waandishi wa Vitabu vya Kiswahili Nchini Kenya". *Nordic Journal of African Studies*, Juz. Na. 15(2):143- 153.

Komakech, R.A. na Magara, E. (2018) "Managing Collaboration between the Author and Publisher for Career Growth in Africa". Katika *Building Capacity for Sustainable Academic and Non-Fiction Authorship in Africa*. Kampala: UTANA. kur 128-136.

Kumar, V.V. (2020) *An Introduction to Self Publishing.* Kottayam: Vimal Kumar V.

Madumulla, J.S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi na Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publisher Ltd.

Makotsi, R. (h.t.) Africa Publishing and Opportunities. Inapatikana katika https: www.Scribd.com. Ilisomwa tarehe 10 Novemba 2025.

Mulokozi, M.M. (1983/2003) "Maendeleo na Matatizo ya Uchapishaji wa Vitabu vya Kiswahili." Katika TUKI. *Uandishi na Uchapishaji: Makala ya Semina ya Kimataifa ya Uandishi wa Kiswahili II*. Dar es Salaam: TUKI. kur.128-141.

Mulokozi, M.M. (Mh.) (1999) *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI. *Uandishi na Uchapishaji.* Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M. (2010) "A Survey of Kiswahili Literature: 1970-1988." *Africa Focus*, Juz. Na. 8(1): 2-13.

Mulokozi, M.M. (2014) *Utangulizi wa Uchapishaji wa Kiswahili na Mchakato wa Uchapishaji* (Kitini cha Uchapishaji) Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M. na Kitogo, S. (Wah.) (2021) 'Barua na Nyaraka za Shaaban Robert II 1926-1962.' (Mswada). Dar es Salaam. TUKI.

Mulokozi, M.M. (2024) "Kiswahili na Uandishi, Uchapishaji na Usomaji Nchini Tanzania". Kiswahili, Juz. Na. 87(2): 220-235.

Ngugi, P.M.Y., Lyimo, E.B. na Bakize, L.H. (2019) *Fasihi ya Kiswahili ya Watoto: Maendeleo, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: TUKI.

Noromba, L. (2007) *Swahili-Literaturliste. Primarliteratur* (hmj) (hm).

Ondari-Okenwa, E. (2007) "Scholarly Publishing in Sub-Saharan Africa in 21st. Century: Challenges and Opportunities". DOI: 10.5210/fm.v12i10.1966.

Osadci-Baciu, A. na Zbuchea, A. (2023) "Beyond Manuscript: Unravelling Author-Publisher Dyanamics". *Culture Society Economy Politics*, Juz. Na. 3(2): 62-80.

Oyeyinka, O.T., Aganbi, V.Em., OdunkuleAdebyo, A. (2016) "Problems of Book Publishing Industry in Nigeria." *Journal of Research and Development*, Juz. Na. 2(10): 1-8.

Phillips, A. na Clark, G. (2025) *Inside Book Publishing.* London: Routledge

Rastogi, M., Rastogi, V. na Rajpoot, D.S. (2024) "Inellectual Property Challenges in Cross Border Business". *International Journal of Multidisciplinary Research*, Juz. Na. 3(6).

Reuster-Jahn, U. (2008) "Newspaper Serials in Tanzania: The Case of Eric James Shigongo (With an Interview)". *Swahili Forum,* Na. 15(2008): 25-50.

Reuster-Jahn, U. (2017) "The Growing Use of Internet for Publishing of Swahili Fiction in Tanzania". DOI: 10.3917/kart.baumg. 2017.01.0269. Ilisomwa tarehe 01 Desemba 2025.

Reuster-Jahn, U. (2020) "The Innovative Transformation of Self-Help Project by Tanzanian Novelists into a Powerful Literary Space." Katika S. Gehrmann,

O. Musumba, O. Obura na J. Ogone (Wah.) *Emerging Trends in Eastern African Literatures and Cultures.* Glienicke: Galda Verlag. kur. 267 – 288.

Robert, S. (1991/2018) *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Rodgers, E.M. (2003) *Diffusion of Innovation*. New York: Free Press.

Ronning, H. (2009) "The Politics of Corruption and Media in Africa". *Journal of African Media Studies,* Juz. 1(1): 155-171. DOI: 10.1386/jams.1.1155.1. Ilisomwa tarehe 20 Novemba 2025.

Schroff, S. (2024) "Missing the Point – the Disappointed Hope of Self Publishing Authors". Inapatikana katika https://doi.org/10.1080/10286632.2023.2288584. Ilisomwa tarehe 15 Oktoba 2025.

Suriano, M. (2021) "Dreams and Constraints of an African Publisher: Walter Bgoya, Tanzania Publishing House and Mkuki na Nyota 1972-2020". *Journal of African Cultural Studies,* Juz. Na. 91(4):575-601.

Timammy, R. na Habwe, J. (2022) "Ushairi wa Simu Tamba na Waswahili wa Pwani ya Kenya." *Kiswahili*. Juz. Na. 85(2): 198-213.